

International Training Program (ITP)

## On-site Education of Practical Languages for Area Studies

### Report in 2011

—kiswahili, University of Nairobi, Kenya, 11 Oct. 2011 –Dec 7. 2010—

Year of Enrollment: 2011

Graduate School of Asian and African Area studies

Tomoko YAGI

#### **On My Language Training**

Mwezi wa nane na watisa, mwaka 2011, nilifanya utafiti katika Mtaa wa Kirisi, Wilaya ya Mwanga, Mkoa wa Kilimanjaro, Tanzania. Mwalimu wangu vile alifanya kazi yake sehemu hiyo.

Wakati wa kipupwe, Mtaa wa Kirisi una matatizo makubwa ya uhaba wa maji. Ingawa ni karibu na mto, hakuna maji ya kutosha, na wakulima wanazimikia kumwagilia mazao kwa kutumia ndoo. Uhaba wa maji unawafanya wakulima washindwe kupata mazao ya kutosha. Mara kwa mara, serikali ya wilaya Mwanga inalazimia kuomba masaada ya vyakula kutoka makao makuu ya mkoa wa Kilimanjaro.

Wakulima wameanza kufanya aina mbali mbali za kazi. Kwa mfano, kutengeneza matofali, kuchonga mawe, ama kuhamia mijini ili kujitafutia kazi.

Kinachonishangaza ni kwa nini kazi nzito ya kuchonga mawe inafanywa na wanawake. Natazamia kwamba wanawake, watoto wazee wamebaki kijijini kwa sababu vijana wamekwenda kutafuta kazi mijini ili kuongeza kipato cha familia.

Wakati huu, sikuweza kufanya utafiti juu ya uchumi wa familia kwa undani. Nikipata bahati ya kurudi tena Wilayani Mwanga, nitaka kufanya utafiti wa jinsi uhaba wa maji unavyoathiri mapato na matumizi ya familia na jinsi wanavyochangua kazi zao.